



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

KUSOGEZWA MBELE KWA TAREHE YA KUTANGAZWA MAJINA YA WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA AWAMU YA PILI YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2020/2021

Dar es Salaam, 24 Oktoba, 2020

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wote wa Elimu ya Juu nchini kuwa Awamu ya Pili ya udahili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2020/2021 ilifungwa tarehe 18 Oktoba, 2020. ***Majina ya waliodahiliwa katika Awamu ya Pili yatatangazwa na vyuo husika tarehe 29 Oktoba, 2020*** badala ya tarehe 24 Oktoba, 2020 iliyokuwa imetangazwa hapo awali. Lengo ni kutoa muda wa kutosha kwa vyuo kukamilisha taratibu za kuchakata na kuidhinisha maombi ya udahili yaliyopokelewa vyuoni katika Awamu ya Pili.

Aidha, ***waombaji ambao walidahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Kwanza na bado hawajakamilisha uthibitisho wao, watapewa utaratibu mwingine wa kujithibitisha na hakuna mwombaji atakayekosa udahili kwa sababu ya kushindwa kujithibitisha.***

Tume inawaasa waombaji wote ambao hawajaweza kutuma maombi ya udahili katika Awamu ya Kwanza na ya Pili kutokana na sababu mbalimbali, wawe na subira na watapewa maelekezo mahususi ya kuzingatia.

Imetolewa na

Dkt. Kokuberwa Katunzi-Mollel
Kny: **KATIBU MTENDAJI**
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA